

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

MUONGOZO WA UENDESHAJI WA VIKUNDI

Imeandaliwa na: Idara ya maendeleo ya Jamii - Kyela

Halmashauri ya Wilaya Katika suala zima la uwezeshaji wananchi kiuchumi, serikali imejipanga kufanya kazi kwa karibu na Vikundi vya wanawake, na vikundi vya vijana, vikundi vya VICOBA na vikundi vya kijamii pamoja na, vyama vya ushirika (SACCOS): kwa mantiki hii tunaona moja kwa moja kwamba, serikali imejipanga kufanya kazi na makundi mbali mbali katika jamii ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Aidha, tuangalie kwa nini serikali na wadau wa maendeleo wanataka kufanya kazi na vikundi au ushirika.

- i. Wananchi wengi wahitaji, hawana dhamana za umiliki wa nyumba ama mashamba ama mali za thamani, katika taasisi za fedha ili wakopesheke, hasa vijana na wanawake, hivyo kupitia vikundi wananchi wanaweza kukopesheka na kikundi kuwa dhamana ya mikopo
- ii. Vikundi ni njia rahisi ya kutiririsha elimu, kwani unaweza kutoa elimu kwa mwanachama mmoja au wawili nao wakaipeleka katika kikundi chote chenye hata zaidi ya watu 30, na hivyo elimu kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi
- iii. Vikundi ni njia rahisi ya kutengeneza mifumo ya kibenki, kama utamaduni wa kuweka akiba, na pia kupata mikopo kwa njia rahisi na masharti nafuu kuliko ya kwenye taasisi mbalimbali za kifedha.
- iv. Kikundi ni njia rahisi ya kufarijiana
- v. Kikundi ni njia rahisi ya kubadilishana uzoefu nk.

Hivyo basi tuangalie kikundi ni nini?

Kikundi ni muunganiko wa watu, wasio ndugu wa karibu, ambao kwa hiyari yao wameamua kujiunga na kuunda kikundi, na wanafanana kwa baadhi ya yafuatayo:- makazi, mahitaji, malengo, shughuli ama itikadi nk.

Kwa mujibu wa mipango na miongozo mbalimbali, ikiwemo,

- Rasimu ya mpango wa milioni 50 kwa kila kijiji ya mwaka 2016, unalenga kufanya kazi na vikundi vilivyosajiliwa aidha ngazi ya wilaya au taifa.
- Mpango wa usajili wa vikundi kwa ngazi ya wilaya wa mwaka 2016 uliotolewa na TAMISEMI unatoa muongozo wa usajili wa Vikundi ngazi ya Wilaya

- Sheria ya usajili wa mashirika yasiyo ya serikali ya mwaka 2002 inampa mamlaka Afisa Maendeleo ya Jamii W, kuwa msajili ngazi ya Wilaya na Msajili msaidizi ngazi ya Taifa
- Mwongozo wa utakelezaji wa Mkakati wa Uwezesaji wananchi kiuchumi wa mwaka 2016, Februari, umelenga kurasimisha vikundi vyote vya kiuchumi na kijamii.

Kwa pamoja inavitaka vyama vyote vya ushirika, vikundi na taasisi zisizo za kiserikali kuwa na usajili, ambao unaweza kuwa wa ngazi ya wilaya ama ngazi ya mkoa au kitaifa. Hivyo, kupitia miongozo hiyo, Halmashauri ya Wilaya imepewa mamlaka ya kufanya usajili wa vikundi kwa ngazi ya wilaya, usajili ambao utatambulika katika mipaka ya wilaya.

Aidha **taratibu za usajili huu ni kama zifuatazo:-**

- Kikundi lazima kiwe na katiba ambayo imejadiliwa na wanakikundi wote.
- Kikundi kitaandika barua ya kuomba kusajiliwa Kwa mkurugenzi mtendaji Wilaya, S. L. P. 320, kyela. Barua hiyo itapitishwa na Afisa mtendaji wa kata, na pia afisa mtendaji wa kijiji ama Mwenyekiti wa kitongoji kwa maeneo ya mamlaka ya mji mdogo wa Kyela.
- Barua ya kuomba usajili, inapaswa kuambatanishwa na muhtasari wa kujadili katiba na kukubaliana kusajili kikundi, na nakala ya katiba ambavyo kwa pamoja vitawasilishwa kwa afisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata, kwa kata ambazo zina maafisa hao kwa ajili ya ukaguzi wa maombi hayo,
- Na kisha maombi hayo kuwasilishwa Halmashauri ya wilaya (idara ya maendeleo ya jamii), ambako ili kusajiliwa, vikundi vitalipia pesa ya usajili (Tshs. 30,000/=) katika akaunti ya Halmashauri na stakabadhi ya benki (cash deposit slip) itawasilishwa idara ya maendeleo ya jamii na kikundi kitakatiwa stakabadhi ya Halmashauri ya Wilaya, na taarifa za kikundi kuchukuliwa. Cheti cha usajili kitatoka ndani ya wiki moja, na hivyo kikundi kinapokuja kuchukua cheti, ni lazima kije na risiti ya Halmashauri ya Wilaya waliyopewa ili waweze kutambulika na kupewa cheti chao.
 - Vikundi ambavyo vilitambuliwa kwa barua, pia vitatakiwa kufanya utaratibu wa kuja na barua zile, na kupewa vyeti vya usajili, ila pia vitatakiwa kulipia kiasi hichohocho cha fedha (30,000), wao watapunguziwa taratibu za ngazi ya kijiji na kata.
 - Vikundi vya VICOBA vitafuata utaratibu wa kawaida wa usajili ili ngazi za vijiji, kata na Wilaya ziweze kuwatambua na kupata usajili rasmi ngazi ya Wilaya.

Faida za usajili:

- 1. Kukidhi vigezo vya kunufaika na Mfuko wa maendeleo ya wanawake na vijana** katika Halmashauri ya Wilaya. Katika mifuko hii, kila mwaka H/W hutenga fedha za kukopesha vikundi vya wanawake na vijana, mikopo ambayo hurejeshwa kwa mwaka mmoja, kwa riba ya asilimia 10% tu. Vikundi vinavyokopesheka na mifuko hii ni vile vyenye watu watao au zaidi, lakini haipendekezwi kwa vikundi vikubwa au vyenye watu wengi

Vigezo vya kukopesheka katika mifuko hii:-

- i. Mikopo hutolewa kwa vikundi tu, kwani dhamana ya mkopo huu ni kikundi
 - ii. Kikundi kiwe kimeomba mkopo husika kupitia barua ya kuomba mkopo, inayopaswa kuandikwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
 - iii. Barua inapaswa kuambataniswa na muhtasari wenye mahudhurio ya wanachama na saini zao, utakaohibitisha kikundi kimeridhia kuomba mkopo na si matakwa ya mtu mmoja ndani ya kikundi.
 - iv. Kikundi kitatakiwa kuambatanisha mchanganuo wa matumizi ya fedha inayoombwa.
 - v. Kikundi hakitakiwi kuwa miongoni mwa vikundi vinavyodaiwa mikopo ya miaka ya nyuma iliyotolewa chini ya mifuko husika.
 - vi. Kikundi kinapaswa kuwa na historia nzuri katika usimamizi wa fedha za kikundi, ikiwemo mfumo mzuri wa kukopeshana na kurejesha ndani ya kikundi
 - vii. Kikundi au mwana kikundi mmoja mmoja anapaswa/wanapaswa kuwa na mradi utakaowezesha kikundi kurejesha fedha wanazotarajia kukopeshwa. na hili litaonekana katika mchanganuo wa mradi unaoombewa kama itakavyoambatanishwa na barua ya maombi ya mkopo, ama itakavyoonekana katika ziara itakayofanywa na wataalam kutembelea miradi ya kikundi
- 2. Kukidhi vigezo vya kukopesheka katika benki ya Posta.** Baraza la uwezeshaji wananchi kiuchumi , limeingia mkataba na benki ya posta, ili benki hiyo iweze kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na SACCOS.

3. **Kukidhi vigezo vya kufungua akaunti benki.** Kwamba, ili kikundi kifungue akaunti benki, taasisi hizo huwa zinahitaji uthibitisho wa kutambulika kwa kikundi husika katika Halmashauri ya Wilaya, ambapo uthibitisho huo hutolewa kupitia cheti cha usajili au barua ambayo hutolewa na H/W kama kikundi kimekamilisha taratibu za usajili.

4. **Kukidhi vigezo vya kunufaika na bodaboda scheme:** huu ni mpango ambao Baraza wameingia mkataba na NSSF ili wawakopeshe vijana waendesha bodaboda pikipiki ili nao waweze miliki za kwao, wainuke kiuchumi, na kukua kimtaji. Mpango huu unataka vijana wa bodaboda kuwa na SACCOS yao ambayo itatakiwa kuwa mwanachama wa NSSF, na wanachama kuwa wanachama wa NSSF ili waweze kukopesheka. Mkopo huu una riba ya asilimia 12.3% kwa muda wa miaka miwili.
 - a. Katika hili, wito unatolewa kwa vijana waendesha bodaboda, ambao tunatambua wana umoja wao, wawe na nia madhubuti ya kuanzisha SACCOS ambayo kupitia hiyo wataweza kupata mikopo hiyo.
Eidha, vijana wa boda boda wanaweza kuamua kujiunga katika SACCOS teule ya vijana Kyela inayoitwa Kyela SACCOS, ambayo kama itaridhiwa kuwa hivyo, tutaitambulisha SACCOS hiyo na kuweza kupata mikopo hiyo kupitia hapo.